SEHEMU YA NNE
SHUGHULI ZA BUNGE

Mpangilio wa Shughuli za Bunge

23.-(1) Rais aweza kulihutubia Bunge siku yoyote ambayo Bunge linakutana.

(2) Wakati wa kuanza kikao cha Mkutano wowote wa Bunge, baada ya Dua kusomwa na Spika kukalia kiti chake:-

(a) Kama Spika amepata taarifa kuwa Rais anakusudia kulihutubia Bunge siku hiyo, Spika atalitangazia Bunge ni wakati gani Rais atafanya hivyo.

(b) Wakati uliopangwa kwa ajili ya Rais kulihutubia Bunge utakapofika, Spika atampokea Rais na kumkaribisha alihutubie Bunge.

(c) Baada ya hotuba ya Rais, Spika aweza ama kusimamisha kikao kwa muda ili kumwezesha amsindikize Rais, au kutaka hoja itolewe ya kuahirisha Bunge hadi siku nyingine itakayotajwa.

(3) Baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Spika atatenga muda kwa ajili ya kujadili hotuba ya Rais.

(4) Shughuli za Bunge katika kila kikao zitaendeshwa kwa mpangilio ufuatao:-

(a) Kuwaapisha Wabunge wapya kiapo cha uaminifu;
(b) Taarifa ya Rais;
(c) Taarifa ya Spika;
(d) Kuwasilisha maombi;
(e) Hati za kuwasilisha Bungeni;
(f) Maswali ambayo taarifa zake zimetolewa;
(g) Hoja za kuahirisha shughuli ili kujadili mambo muhimu ya dharura;
(h) Kauli za Mawaziri;
(i) Maelezo binafsi ya Wabunge;

(j) Mambo yahusuyo haki za Bunge;
(k) Shughuli za Serikali;
(l) Hoja au taarifa za Kamati;
(m) Hoja binafsi za Wabunge.

(5) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Kanuni hii, katika kila Mkutano wa Bunge, Spika atatenga muda mahsusi kwa ajili ya Bunge kushughulikia hoja binafsi za Wabunge na Miswada binafsi ya Wabunge, kama itakuwapo.

(6) Shughuli za Bunge katika kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata jinsi zilivyowekwa katika Orodha ya Shughuli za siku hiyo, na kwa kufuata utaratibu mwingine ambapo Spika ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

(7) Serikali itakuwa na haki ya kuagiza Shughuli zake ziwekwe katika Orodha ya Shughuli kwa mpangilio ambao Serikali itaupendelea.

Dua

24. Dua iliyowekwa na Bunge itasomwa na Spika au Katibu, kadri itakavyokuwa.

Kiapo cha Uaminifu

25.-(1) Kiapo cha Uaminifu kilichowekwa na Kanuni hii kitaapishwa kwa kila Mbunge; lakini Mbunge aweza, kabla ya kuapa kiapo hicho, kushiriki katika uchaguzi wa Spika.

(2) Mbunge yeyote aliyechaguliwa kuwa Spika kabla ya kushika madaraka yake, ataapa Kiapo cha Spika mbele ya Bunge. Lakini endapo atachaguliwa Spika ambaye siyo Mbunge, basi ataapa Kiapo cha uaminifu kwanza kabla ya kuapa Kiapo cha Spika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (4), maneno yafuatayo ndiyo yatakuwa Kiapo cha Uaminifu:-

"Mimi (Mbunge atataja jina lake), naapa kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote, na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na nitaitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie."

(4) Iwapo Mbunge yeyote haamini kuwa kuna Mungu, aweza kuapa Kiapo cha Uaminifu kuacha maneno "Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie."

Taarifa ya Rais

26.-(1) Taarifa ya Rais, kama ipo, itasomwa na Spika au Waziri.

(2) Kila inapowezekana, taarifa ya Rais itasomwa Bungeni wakati jambo la (b) la "Shughuli za Bunge", zilivyowekwa na Kanuni ya 23(4) litakapofikiwa; lakini Spika aweza, wakati wowote, kusimamisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kuwezesha taarifa hiyo isomwe.

Taarifa ya Spika

27.-(1) Spika atatoa taarifa kuhusu Miswada yote iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wake uliotangulia, yaani kama imekubaliwa na Rais au kama Rais ametoa uamuzi mwingine.

(2) Spika aweza kutoa taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa.

Kuwasi-lisha Maombi

28.-(1) Mbunge yeyote aweza kuwasilisha Bungeni maombi yoyote juu ya jambo lolote kwa niaba ya watu wanaotoa ombi hilo, na halitatolewa Bungeni mpaka kwanza taarifa ya ombi hilo iwe imetolewa kwa maandishi na kupokelewa na Katibu si chini ya siku mbili za kazi kabla ya Mkutano ambapo ombi hilo linakusudiwa kutolewa.

(2) Ombi lolote laweza kuwasilishwa, Bungeni na Mbunge tu, likionyesha dhahiri jina la Mbunge anayeliwasilisha.

(3) Mbunge anayewasilisha ombi atatoa maelezo mafupi ya kutambulisha watu wanaotoa ombi hilo, idadi yao, saini zilizoambatanishwa kwenye ombi hilo, madai ya msingi yaliyomo, na madhumuni ya ombi hilo.

(4) Baada ya kutimiza masharti ya fasili ya (3), Mbunge anayewasilisha ombi aweza kutoa hoja kwamba, Bunge lijadili ombi hilo. Hoja hiyo, haihitaji kutolewa taarifa na itaamuliwa bila mjadala wowote. Hoja ya kujadili ombi ikikubaliwa, itashughulikiwa kwa kufuata mpangilio wa shughuli uliowekwa, na Kanuni ya 23(4).

(5) Mbunge yeyote hataruhusiwa kuwasilisha ombi linalomhusu yeye mwenyewe au ambalo yeye amelitia saini yake, au ambalo linakiuka masharti ya Kanuni ya 77.

Masharti kuhusu Maombi

29. Ombi lolote halitawasilishwa Bungeni isipokuwa tu kama Spika ataridhika kuwa limezingatia masharti yafuatayo:-

(a) Limeandikwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza; au
(b) Limeandikwa kwa lugha ya heshima na taadhima na linamalizia kwa maelezo ya jumla kuhusu madhumuni ya ombi hilo.

Taarifa ya Kuwasilisha maombi

30. Nakala ya kila ombi itawasilishwa kwa Katibu siku zisizopungua mbili kabla ya siku ya kuwasilishwa Bungeni.

Hati za kuwasilishwa Bungeni

31.-(1) Hati zaweza kuwasilishwa Bungeni wakati wa vikao vyake:-

(a) na Waziri;
(b) na Mbunge asiyekuwa Waziri.

(2) Iwapo Bunge haliko katika kikao, kwa kuziwasilisha kwa Katibu pamoja na barua iliyotiwa saini na Waziri mwenyewe au Katibu Mkuu wake au na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; au na Mbunge anayehusika; na kumbukumbu ya hati zote zilizowasilishwa Bungeni zitaingizwa katika Taarifa Rasmi.

(3) Hati zote zitawasilishwa Bungeni bila kutolewa hoja yoyote kwa ajili hiyo.

(4) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake, zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri. Hakutatakiwa kutolewa taarifa ya kuwasilisha hati hizo.

(5) Mbunge yeyote atakuwa na haki, endapo atamuomba hivyo Katibu, wakati wowote unaofaa, kusoma na, kama anataka hivyo, kunukuu sehemu, au kupata nakala ya hati zote zilizowasilishwa Bungeni.

Kujadili Hati zilizowa-silishwa

32.-(1) Wakati wowote baada ya hati yoyote kuwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 31, Waziri au Mbunge aliyewasilisha hati hiyo, au Mbunge mwingine yeyote, aweza kutoa hoja kwamba Bunge lijadili hati hiyo. Hoja inayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii haitahitaji kutolewa taarifa, na itaamuliwa bila mabadiliko au mjadala wowote. Hoja ya kujadili hati iliyowasilishwa Bungeni ikikubaliwa, itashughulikiwa kwa

kufuata masharti ya Kanuni ya 23(4). Isipokuwa kwamba taarifa zinazowasilishwa Bungeni na Kamati yoyote ya Kudumu, au na Kamati Teule, zitatengewa muda wa kujadiliwa Bungeni bila hoja kutolewa.

(2) Mjadala unaweza kugusia kila jambo lililomo katika hati na itajadiliwa aya kwa aya, isipokuwa kama Spika, kwa kuzingatia uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, ataamua vinginevyo.

Maswali

33.-(1) Waziri anaweza kuulizwa maswali kuhusu masuala yoyote ya umma au jambo lingine lolote ambalo linasimamiwa na Waziri au Ofisi yake. Vile vile Mbunge yeyote aweza kuulizwa maswali kuhusu mambo yoyote anayohusika nayo kutokana na kuteuliwa na Bunge kushughulikia mambo hayo.

(2) Madhumuni halali ya swali lolote yatakuwa ni kutaka kupewa habari kuhusu jambo mahsusi ambalo kwalo Waziri, au Mbunge anayehusika anawajibika, au kutaka kusisitiza hatua fulani zichukuliwe au wajibu utekelezwe.

Taarifa za Maswali

(3) Taarifa ya swali itakuwa katika maandishi na itapelekwa na kumfikia Katibu si chini ya siku ishirini na moja kabla ya tarehe ambayo jibu litahitajiwa litolewe, lakini taarifa haitatolewa Bungeni kwa mdomo tu Taarifa zote za maswali zitakazoruhusiwa na Spika zitaingizwa katika Kitabu cha Shughuli za Bunge kuonyesha kuwa zimepokelewa. Maswali yote yaliyopangwa kujibiwa siku fulani, yatawekwa katika Orodha ya Shughuli za siku hiyo.

Endapo swali halikuwahi kujibiwa siku hiyo kwa sababu ya muda wa maswali kumalizika, litapangiwa nafasi ya kujibiwa baadaye katika Mkutano huo unaoendelea. Kama siku inayohusika ndiyo siku ambapo mkutano wa Bunge unafungwa, swali hilo litajibiwa katika mkutano unaofuata. Bunge linapovunjwa, maswali yote ambayo hayakuwahi kujibiwa yatakuwa yamefutwa, lakini yaweza kuulizwa tena katika Bunge linalofuata, baada ya kutolewa taarifa mpya.

(4) Kwa kawaida, maswali yatajibiwa Bungeni kwa mdomo. Lakini endapo Mbunge mwenye swali hayupo Bungeni kuuliza swali lake, na Spika hakutoa ruhusa kwa swali hilo kuulizwa na Mbunge mwingine aliyehudhuria. kwa niaba ya Mbunge huyo wa kwanza, basi Waziri aliyeulizwa swali atapeleka kwa Katibu jibu la maandishi naye Katibu ataliingiza jibu hilo

katika Taarifa Rasmi. Mbunge yeyote hatauliza zaidi ya maswali manne yanayohitaji majibu ya mdomo katika Mkutano mmoja isipokuwa katika Mkutano wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali.

(5) Maswali yote katika Mkutano mmoja yatapewa nambari zinazofuatana kwa mfululizo na nambari zilizotolewa kwa kila swali zitaingizwa katika Kitabu cha Shughuli za Bunge, Orodha ya Shughuli na katika Taarifa Rasmi, lakini maswali yote ambayo yamepangwa kujibiwa na Waziri, au na Mbunge mwingine katika kikao kimoja, yanaweza kuwekwa pamoja katika Orodha ya Shughuli na kujibiwa kwa zamu na Waziri au na Mbunge anayehusika kadri itakavyoonyeshwa katika Orodha ya Shughuli.

Masharti Kuhusu Maswali

34.-(1) Maswali yaweza kuulizwa endapo masharti yafuatayo yatazingatiwa:-

(a) Swali halitamtaja mtu yeyote kwa jina au kutoa maelezo yoyote mahsusi, ila tu kama ni lazima kabisa ili kulifanya swali lieleweke;

(b) Endapo swali lina maelezo yoyote mahsusi Mbunge anayeuliza swali hilo atawajibika kuhakikisha kuwa maelezo hayo ni sahihi, lakini madondoo kutoka katika hotuba, vitabu au magazeti hayatakubaliwa;

(c) Swali halitakuwa kisingizio cha kufanya mjadala, na Mbunge hatalihutubia Bunge kuhusu jambo analoliuliza;

(d) Swali halitahusu mambo zaidi ya moja, na lisiwe refu kupita kiasi;

(e) Swali halitakuwa namna ya hotuba fupi, au kuwa tu na madhumuni ya kutoa habari, au kuulizwa kwa njia inayoonyesha jibu lake au kutambulisha mkondo fulani wa maoni;

(f) Swali lisiwe na maelezo ya dhihaka, maoni, masingizio, sifa zisizolazimu; au kutegemea habari za kubahatisha tu;

(2) Swali lolote halitaruhusiwa kuulizwa:-

(i) Kama linakiuka Kanuni yoyote ya Bunge;

(ii) Kama limekusudiwa kupata maoni, au utatuzi wa tatizo la kisheria, la kinadharia au kutoa mapendekezo juu ya jambo la kubahatisha tu;

(iii) Kama linaanzisha upya jambo ambalo limekwisha kuamuliwa Bungeni, au ambalo limejibiwa kwa ukamilifu katika Mkutano uliopo au uliotangulia huo uliopo, au ambalo limekataliwa kujibiwa;

(iv) Kama linataka habari juu ya mambo ambayo kwa namna yake ni siri zinazohusiana na ulinzi au usalama wa Taifa;

(v) Kama linahusu Shughuli za Kamati ya Bunge ambayo haijawasilishwa Bungeni kwa taarifa ya Kamati hiyo, au ambayo Spika hajaarifiwa kuwa Kamati imemaliza kuyashughulikia;

(vi) Kama linahusu mambo ambayo yamepelekwa kwa Kamati ya Uchunguzi;

(vii) Kama linahusu tabia au mwenendo wa mtu yeyote ila tu kama ni kuhusu mtu huyo katika kutekeleza wajibu wake kama mtumishi wa umma;

(viii) Kama linahusu jambo lolote ambalo wakati huo liko mbele ya Mahakama, au kama lina madbumuni ya kuchunguza uamuzi uliokwisha kutolewa na Mahakama;

(ix) Kama linashutumu tabia au mwenendo wa mtu yeyote ambaye mwenendo wake waweza tu kukabiliwa kwa hoja maalum iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(6);

(x) Kama linahitaji habari ambazo zinapatikana katika hati ambazo Mbunge anaweza kujisomea mwenyewe kama vile nakala za Sheria au maandiko ya kumbukumbu za kawaida;

(xi) Kama linahitaji mambo ya sera ambayo ni makubwa mno kiasi cha kutoweza kujibiwa sawa sawa kwa kuzingatia taratibu za kujibu maswali;

(xii) Kama linauliza iwapo usemi wa binafsi au wa vyombo visivyo vya Serikali ni sahihi au si sahihi.

Jinsi ya Kuuliza Maswali

35.-(1) Wakati swali linalohitaji jibu la mdomo litakapofikiwa katika Orodha ya Shughuli, Spika atarnwita Mbunge ambaye swali hilo limeandikwa pamoja na jina lake au, kama Spika arnekubali, Mbunge aliyeruhusiwa kuuliza swali hilo kwa niaba ya Mbunge ambaye swali limeandikwa pamoja na j ina lake, Mbunge atakayeitwa. atasimama mahali pake na kuuliza swali kwa kutaja nambari ya swali hilo iliyopo katika Orodha ya Shughuli, na Waziri, au Mbunge aliyeulizwa swali papohapo, atatoa jibu lake; lakini maswali aliyoulizwa Waziri mmoja yaweza kujibiwa na Waziri mwingine au, kwa idhini ya Spika, na Mbunge mwingine aliyeidhinishwa na Waziri.

(2) Katika Mkutano wa Bajeti, swali lolote halitaulizwa Bungeni baada ya kupita muda wa saa moja tangu Bunge lilipoanza shughuli za maswali. Katika mikutano mingine yote, baada ya kupita saa moja na nusu.

(3) Spika aweza kuweka kiwango cha juu cha maswali yatakayowekwa katika Orodha ya Shughuli ambayo anaona yanaweza kujibiwa katika muda uliowekwa.

(4) Mbunge, anayeuliza swali aweza kuliondoa swali lake wakati wowote kabla halijajibiwa, ama kwa kumpa Katibu taarifa kwa maandishi, au kwa Mbunge huyo kusimama mahali pake jina lake linapoitwa wakati wa maswali na kusema kuwa analiondoa swali lake.

Maswali ya Nyongeza

36.-(1) Maswali ya nyongeza yaweza kuulizwa na Mbunge yeyote kwa madhumuni ya kutaka kueleweshwa zaidi juu ya jambo lolote lililotajwa katika jibu lililotolewa. Masharti ya Kanuni ya 34(l) yatatumika pia kwa maswali ya nyongeza.

(2) Mbunge anayeuliza swali la msingi ataruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza yasiyozidi mawili. Lakini Mbunge mwingine yeyote atakayepewa nafasi ataruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa madhumuni ya Kanuni hii, swali ambalo litawekwa katika vifungu vya (a) na (b) litahesabiwa kuwa ni maswali mawili.

(3) Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, Wabunge

watakaouliza maswali ya nyongeza hawatazidi watatu kwa swali moja la msingi, na Mbunge hataruhusiwa kusoma swali lake.

Masharti kuhusu maswali ya Nyonge-za

37.-(l) Spika hataruhusu swali lolote la nyongeza ambalo linaleta mambo yasiyotokana au kuhusiana na lile la msingi, an kama linakiuka yale masharti yaliyoainishwa katika Kanuni ya 34(l) yanayohusu taratibu za kuuliza maswali.

(2) Endapo Spika atakataa swali la nyongeza kwa kukiuka masharti ya Kanuni ya 34(l); swali hilo halitajibiwa, na halitaonyeshwa, katika Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge.

Mawazi-ri kujibu maswali kwa ukamili-fu

37A.-(1) Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa. Isipokuwa kwamba kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampatia muuliza swali nakala ya jibu hilo mapema baada ya kikao kuanza, kabla swali hilo halijafikiwa kujibiwa.

(2) Waziri aweza, akiombwa na muuliza swali anayehusika, kumpatia rasimu ya jibu la swali lake mapema baada ya kikao kuanza, kabla swali hilo halijafikiwa kujibiwa.

(3) Waziri yeyote mwingine aweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri mwenzake.

Kuahiri-sha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura

38.-(1) Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote aweza kutoa hoja kuwa Bunge liahirishe shughuli zake kama zilivyoonyeshwa katika Orodha ya Shughuli, ili lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(2) Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na haitatolewa wakati majadiliano yanaendelea kuhusu jambo jingine.

(3) Hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahali pake na kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma, isipokuwa kama dharura inayohusu itakuwa imetokea muda huo huo, itabidi Mbunge mtoa hoja awe amewasilisha kwa Spika kwa maandishi, maelezo ya jambo analopenda lijadiliwe, kabla ya kikao kuanza.

(4) Endapo Spika ataliona jambo hilo ni la dharura, ni halisi na la muhimu kwa umma, ataruhusu hoja hiyo itolewe; na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda usiozidi nusu saa.

38A.-(1) Masharti ya jumla yafuatayo yatatumika vile vile kuhusu hoja iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii, yaani:-

(a) Hoja hiyo haitaruhusiwa iwapo inahusu jambo ambalo kwalo taarifa ya hoja imekwisha kutolewa au jambo ambalo limekwisha kuwekwa katika Orodha ya Shughuli;

(b) Hakutaruhusiwa hoja zaidi ya moja katika kikao kimoja zenye kutaka kuahirisha Shughuli za Bunge kwa kutumia Kanuni hii;

(c) Jambo ambalo litakuwa limejadiliwa katika hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii, halitaletwa tena Bungeni katika Mkutano ule ule kwa kutumia Kanuni hii.

(2) Jambo linaloletwa kwa hoja chini ya Kanuni hii litahesabiwa tu kuwa ni jambo halisi iwapo:-

(a) Ni jambo moja mahsusi;

(b) Halikuwekwa katika lugha ya jumla an haligusi mambo mengi mbalimbali;

(c) Haliletwi kwa kutegemea habari zisizo za hakika au habari halisi juu ya jambo hilo hazipatikani;

(d) Linahusu mambo ya kinadharia tu.

(3) Jambo linaloletwa kwa hoja chini ya Kanuni hii litahesabiwa kuwa ni jambo la dharura iwapo:-

(a) Ni wazi kabisa kwamba ni jambo la dharura;

(b) Limetokea siku hiyo au jana yake, na limeletwa bila kuchelewa;

(c) Hakutatokea fursa ya kulijadili siku za karibuni kwa njia ya kawaida ya kushughulikia mambo ya Bunge.

(4) Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni la muhimu kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa sheria peke yake.

Kauli za Mawaziri

39.-(1) Waziri aweza kutoa kauli Bungeni kuhusu jambo lolote ambalo kwalo Serikali inawajibika.

(2) Kauli za aina hiyo zaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mfululizo wa shughuli ambao umewekwa na Kanuni ya 23(4). Muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini.

Maelezo binafsi ya Wabunge

40. Mbunge yeyote aweza, kwa kibali cha Spika, kutoa maelezo yake binafsi Bungeni chini ya Kanuni hii. Lakini Mbunge anayekusudia kufanya hivyo atapaswa kuwasilisha maelezo yake hayo maperna kwa Spika. Spika akiridbika kwamba maelezo hayo hayakiuki Kanuni yoyote ya Bunge, atarubusu yatolewe kwa kusomwa Bungeni. Muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi kumi na tano.

Masuala yanayohusu Haki za Bunge

41.-(1) Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mfululizo wa shughuli uliowekwa na Kanuni ya 23(4) na atakuwa amemwarifu Spika mapema kuhusu kusudi lake hilo, na jambo ambalo anataka kuliwasilisha.

(2) Spika akimwita, Mbunge ataeleza kwa kifupi sababu zinazofanya aamini kwamba jambo analoliwasilisha linahusu haki za Bunge zilizotajwa katika Sheria Na.3 ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya 1998.

(3) Baada ya hapo Spika ataeleza kama kwa maoni yake jambo hilo linahusu au halihusu haki za Bunge. Endapo atakubali kuwa jambo hilo linahusu haki za Bunge, basi Mbunge mhusika atatoa hoja yake kuhusu jambo hilo, na hoja hiyo itapewa nafasi muhimu ya kutangulia shughuli nyingine zote za kikao kinachobusika.

(4) Mambo yanayohusu haki za Bunge yatawasilishwa kwa kufuata

utaratibu uliowekwa katika Kanuni ya 23 (4), lakini endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge jambo lolote litazuka ghafla ambalo linaonekana kama linahusu haki za Bunge, isipokuwa tu kama wakati huo kura inapigwa, shughuli zitasimamishwa kwa madhumuni ya kuliwezesha jambo hili kuwasilishwa na kuamuliwa.

Shughuli za Serikali

42.-(1) Shughuli za Serikali ni zile ambazo zitawasilishwa Bungeni na Waziri, au na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(2) Shughuli za Serikali zitaanza wakati Spika atakapomwita Waziri aliyetoa taarifa ya kuwasilisha Muswada au ya kutoa hoja Bungeni, baada ya Katibu kusoma jambo linalohusika katika Orodha ya Shughuli.

(3) Baada ya Spika kutoa wito huo, Mbunge yeyote binafsi hawezi tena kutoa hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 38, vile vile hawezi kuuliza swali.

43.-(1) Isipokuwa kama Kanuni hizi zimeagiza vinginevyo, hakuna. mjadala wowote utakaoendeshwa Bungeni ila tu kuhusu shughuli iliyoingizwa katika Kitabu cha Shughuli za Bunge na kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli.

Hoja Bungeni

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba na ya Kanuni hizi, Waziri au Mbunge yeyote mwingine aweza, kwa kutoa hoja, kupendekeza kwamba suala lolote lijadiliwe Bungeni; na hoja hiyo itaamuliwa kwa kufuata Kanuni hizi.

(3) Isipokuwa kama Spika ataamua vinginevyo, kila hoja ambayo taarifa yake imekubaliwa, itapelekwa kwanza kwenye Kamati inayohusika.

(4) Endapo hoja itapelekwa kwenye Kamati inayohusika, Kamati hiyo itaanza kuitafakari hoja hiyo mapema iwezekanavyo, na haitatolewa Bungeni mpaka Mwenyekiti wa Kamati hiyo atakapokuwa amemtaarifu Spika kwamba Kamati imemaliza kuitafakari. Kamati iliyopelekewa hoja kwa mujibu wa Kanuni hii haitakuwa na uwezo wa kufanya mabadiliko yoyote katika hoja hiyo.

Lakini kama hoja inayohusika ni hoja binafsi, Kamati yaweza

kumwelekeza mtoa hoja hiyo afanye mabadiliko ambayo Kamati itaona yanafaa, kabla haijawasilishwa Bungeni.

(5) Endapo hoja haikupelekwa kwenye Kamati na imewekwa kwenye Orodha ya Shughuli, au kama ilipelekwa kwenye Kamati na Kamati hiyo imemaliza kuishughulikia na imewekwa kwenye orodha ya Shughuli, hoja itawasilishwa na kuamuliwa Bungeni kwa kufuata masharti yafuatayo:-

(a) Baada ya hoja kutolewa na inapobidi hivyo kuungwa mkono, Spika ataomba hoja hiyo ijadiliwe,

(b) Mara baada ya Waziri au Mbunge mwingine anayehusika kuwasilisha hoja yake, Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa hoja hiyo atatoa maoni ya Kamati yake juu ya hoja hiyo.

(c) Baada ya hapo, kama hoja inayohusika ni hoja ya Serikali, msemaji wa Upinzani atapewa nafasi ya kutoa maoni ya upande wa Upinzani juu ya hoja hiyo; na kama hoja inayohusika siyo hoja ya Serikali, msemaji wa Serikali atapewa nafasi ya kutoa maoni ya Serikali juu ya hoja hiyo. Isipokuwa kwamba masharti ya fasili hii hayahusu hoja za Kamati.

(d) Kama hoja moja inahusu masuala mawili au zaidi, Spika aweza kuomba Bunge liamue masuala yote kwa pamoja au mbalimbali kama itakavyoona inafaa.

(e) Baada ya mjadala kumalizika, kama utafanyika, Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi wa Bunge.

(6) Spika aweza kuweka kiwango cha juu cha muda utakaotumiwa kujadili hoja.

(7) Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kuliamua ama katika Mkutano huo uliopo au ule uliotangulia, isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni ya 44(2).

44.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba au ya Kanuni hizi, Mbunge yeyote aweza kupendekeza jambo lolote lijadiliwe Bungeni kwa kutoa hoja, yaani kwa kutoa pendekezo lililokamilika ili lipate uamuzi wa

Bunge; na itabidi liwe limewekwa, katika lugha ambayo italiwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Kanuni hizi, mfumo wa maneno ya hoja inayowasilishwa Bungeni utakuwa kama ifuatavyo:-

KWA KUWA ----------

NAKWA KUWA ----------
(n.k.)
KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba ----------

(2) Taarifa ya hoja ambayo, kwa maoni ya Spika, ina lengo la kujaribu kutaka lifikiriwe tena jambo ambalo lilikwisha kuamuliwa na Bunge katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyopita kabla ya kikao kinachoendelea, haitakubaliwa na Spika isipokuwa tu kama ni hoja ya kutaka uamuzi wa Bunge uliokwisha kufanyika ubadilishwe.

(3) Taarifa yoyote ya hoja ambayo inakiuka masharti ya Katiba, au ya Kanuni ya 77, haitakubaliwa.

Taarifa ya hoja

45.-(1) Isipokuwa kama Kanuni hizi zitaruhusu vinginevyo, au kama Spika atatoa idhini yake kwa kutilia maanani udharura wa jambo lenyewe, hoja yoyote haitatolewa Bungeni mpaka taarifa ya hoja hiyo iwe imetolewa na kupokelewa na Katibu angalau siku mbili za kazi kabla ya Mkutano ambapo hoja hiyo inakusudiwa kutolewa.

(2) Iwapo, kwa mujibu wa Kanuni hizi, taarifa ya hoja yatakiwa kutolewa, basi taarifa hiyo itabidi itolewe kwa maandishi, itiwe saini na Mbunge anayeitoa na ipelekwe kwa Katibu ili aipokee kufuatana na masharti ya fasili ya (1) ya Kanuni hii; isipokuwa kwamba muda wa chini kabisa wa kutoa taarifa ya hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja iliyotolewa ama Bungeni au katika Kamati ya Bunge Zima, utakuwa ni siku moja ya kazi kabla ya kikao ambapo hoja hiyo ya mabadiliko inakusudiwa kutolewa. Lakini Spika, ama kutokana na dharura au sababu nyingine yoyote itakayomridhisha, aweza kuruhusu hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja inayohusika itolewe bila taarifa.

(3) Hoja zifuatazo zaweza kutolewa bila taarifa, yaani:-

(a) Hoja ya kutengua yoyote kati ya Kanuni hizi;

(b) Hoja ya kuahirisha Bunge au kuahirisha mjadala;

(c) Hoja ya kumsimamisha kazi Mbunge;

(d) Hoja ya kutaka wageni waondoke Bungeni;

(e) Hoja ya kwamba ombi lililowasilishwa Bungeni lijadiliwe;

(f) Hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura;

(g) Hoja kuhusu jambo lolote linalohusiana na haki za Bunge;
(h) Hoja ya kutaka Hati iliyowasilishwa Bungeni ijadiliwe.

(4) Hoja yoyote ambayo kwa dhahiri inahusu haki za Bunge itazitangulia hoja na shughuli nyinginezo zote za siku hiyo. Endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge jambo lolote litatokea ambalo kwa dhahiri linahusu haki za Bunge, basi shughuli nyingine zitasimamishwa, ili Bunge liweze kujadili hoja hiyo, isipokuwa tu kama wakati huo kura inapigwa.

(5) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (2) ya Kanuni hii, iwapo Mbunge anayetoa taarifa ni Waziri, taarifa hiyo yaweza kutiwa saini kwa niaba yake na Katibu Mkuu au na Mwanasheria Mkuu. Endapo hoja ambayo kwayo taarifa iliyotolewa haitajadiliwa katika Mkutano alioutaja Mbunge mtoa hoja, basi taarifa ya hoja hiyo itatenguka, lakini yaweza kutolewa tena.

(6) Taarifa haitaacha kutolewa kuhusu jambo lolote linalohitaji taarifa itolewe kwa mujibu wa Kanuni hizi, isipokuwa tu kwa idhini maalum ya Spika.

(7) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (9), taarifa za hoja zitaingizwa katika Kitabu cha Shughuli mapema baada ya kupokelewa na Katibu, na zitawekwa katika Orodha ya Shughuli ya kikao cha Bunge kulingana na maelekezo ya Spika.

(8) Taarifa zitawekwa katika Orodha ya Shughuli zikiwa kama zilivyoletwa au baada ya kufanyiwa marekebisho au mabadiliko ambayo Spika, kwa kibali cha Mbunge mtoa taarifa, ataagizwa yafanywe; lakini Spika hataruhusu taarifa yoyote ya hoja iwapo inakiuka Kanuni yoyote na

iwapo ataikataa basi Katibu atairudisha taarifa hiyo kwa Mbunge, pamoja na maelezo ya sababu za kukataliwa kwa hoja hiyo.

(9) Iwapo Mbunge anapenda kufanya mabadiliko katika maeneo aliyoyatumia katika hoja anayokusudia kuitoa, aweza kufanya hivyo kwa kutoa taarifa ya kutaka kufanya mabadiliko angalau siku moja kabla ya siku ile ambapo hoja hiyo imewekwa katika Orodha ya Shughuli ili ijadiliwe. Endapo Mbunge atashindwa kutoa taarifa ya hoja ya kutaka kufanya mabadiliko, basi anaweza kuomba ruhusa ya Spika ili afanye mabadiliko katika hoja yake bila ya kutoa taarifa kwanza.

(10) Bila ya kujali kwamba taarifa ya hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja ya awali imetolewa, mabadiliko yoyote hayatakubaliwa kama, kwa maoni ya Spika, mabadiliko hayo yanabadilisha mambo ya msingi yaliyomo katika hoja ya awali au yanabadilisha makusudio au upeo wa hoja hiyo.

Jinsi ya kujadili hoja

46.-(1) Mbunge atakapoitwa na Spika kutoa hoja yake atasimama mahali pake na kutoa hoja yake hiyo.

(2) Kila hoja au mabadiliko katika hoja hiyo ambayo, kwa mujibu wa Kanuni hizi, yanahitaji kuungwa mkono, itatenguka kama haikuungwa mkono, na ikitokea hivyo Katibu ataandika maelezo katika kumbukumbu rasmi kwamba kwa kuwa hoja haikuungwa mkono, Spika hakuweza kuitoa ili ijadiliwe.

(3) Mbunge aweza kuunga mkono hoja kwa kusimama tu mahali pake bila kusema lolote kuhusu hoja hiyo, kisha akakaa; lakini Mbunge aliyefanya hivyo bado atakuwa na haki ya kuizungumzia hoja hiyo hapo baadaye.

(4) Iwapo hoja imewekwa katika Orodha ya Shughuli na Mbunge mtoa hoja anapoitwa na Spika kuitoa anashindwa kuitoa hoja hiyo, hoja itatenguka ila kama Mbunge mwingine aliyeidhinishwa na huyo mtoa hoja ataitoa kwa niaba yake; isipokuwa kama Mbunge huyo ametoa taarifa ya kutaka kuiahirisha; lakini hoja kuhusu shughuli za Serikali yaweza kutolewa na Waziri yeyote au na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(5) Hoja iliyotenguka yaweza kutolewa tena baadaye, baada ya taarifa mpya kutolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(6) Endapo hakuna Wabunge zaidi wanaopenda kuzungumzia hoja iliyotolewa, au endapo muda uliowekwa wa kujadili hoja hiyo kwa mujibu wa Kanuni hizi umekwisha, Spika atampa mtoa hoja nafasi ya kujibu; au, endapo wakati huo Bunge liko katika Kamati ya Bunge Zima likifikiria vifungu vya Muswada wa Sheria; au katika Kamati ya Matunlizi likifikiria vifungu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikah, basi papo hapo Mwenyekiti atawahoji kwa pamoja vifimgu vyote vilivyobaki.

Kubadi-lisha hoja

47.-(l) Hoja ikisha kutolewa ili iamuliwe yaweza kubadilishwa:-

(a) Kwa kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza mancho mengine;

(b) Kwa kuondoa maneno fulani bila kuongeza mengine au;

(c) Kwa kuingiza au kuongeza maneno mapya.

(2) Isipokuwa kama taarifa imetolewa mapema, mtoa hoja ya kubadilisha hoja, kabla ya kutoa hoj a hiyo, atamkabidhi Katibu maandishi yenye saini yake na yanayoonyesha mabadiliko anayotaka yafanywe; lakini Spika anaweza kulegeza shard hili kama mabadiliko yanayokusudiwa ni madogo au ni ya uhariri.

(3) Kila badiliko linalopendekezwa sharti liwiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko na sharti badiliko hilo hungwe mkono na lisfingize jambo lolote ambalo, kwa maoni ya Spika, laweza tu kuwasilishwa kwa hoja maalum baada ya kutolewa taarifa.

(4) Badiliko lolote halitaruhusiwa kama kwa maoni ya Spika, linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa.

(5) Baada ya uamuzi kutolewa kuhusu badiliko katika sehemu yoyote ya hoja, sehemu yoyote inayoitangulia sehemu hiyo katika hoja hiyo haiwezi tena kubadilishwa; hali kadhalika, iwapo hoja ya kubadilisha sehemu yoyote ya hoja imekwisha kutolewa na Spika ili ijadiliwe, sehemu inayotangulia hiyo katika hoja hiyo haiwezi tena kubadilishwa.

(6) Hoja yoyote ya kutaka kufanya mabadiliko haitaruhusiwa kama inapingana na uamuzi wa nyuma uliokwisha kutolewa juu ya suala hilo hilo.

(7) Hoja yaweza kutolewa kwa ajili ya kufanya mabadiliko katika hoja ja mabadiliko mengine iliyotolewa na Spika kwaWabunge ili waijadili.

(8) lwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kuondoa maneno fulani na kuingiza maneno mengine, basi mjadala juu ya suala la kafanya mabadiliko waweza kuangalia kwa pamoja yale maneno yanayopendekezwa yaondolewe na maneno ambayo yanapendekezwa yaingizwe. Iwapo hoja inapendekeza kuondoa au kuingiza maneno, mjadala utahusu tu uondoaji au uingizaii wa maneno mapya, kadri itakavyokuwa.

(9) Hojayakufanyamabadilikokatikahojanyingineyamabadiliko sharti ihusiane na hoja ya kwanza ya mabadiliko; na itatolewa, itajadiliwa na kuamuliwa kabla ya ile hoja ya kwanza ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi.

Jinsi ya Kujadili Mabadi-liko ya Hoja

48.-(l) Endapo Mbunge anapenda kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi aweza kutoa hoja yake ya kufanya mabadiliko wakati wowote baadaya hoja anayotaka kuibadilisha kutolewa, lakini kabla Bunge halijahojiwa hifanyie uamuzi.

(2) Endapo kuna mapendekezo mawili au zaidi ya kubadilisha hoja moja, Spika ataita watoa hoja hizo kwa kufuata mpangilio atakaoamua yeye.

(3) Iwapo mapendekezo yote ya mabadiliko yameamuliwa, Spika ataitoa tena hoja ya awali ili ijadiliwe kama itakavyokuwa imebadilishwa.

Kuondoa Hoja

(4) Hoja yoyote yaweza kuondolewa wakati wowote kabla hoja hiyo haijafikishwa Bungeni, iwapo Mbunge mtoa hoja atamuagiza Katibu hivyo.

(5) Endapo hoja imefikishwa Bungeni, mtoa hoja anaweza tu kuondoa hoja yake kwa kusirnama mahali pake na kusema "Ninaomba ruhusa kaondoa hoja", na papo hapo Spika ataliuliza Bunge kama linaafiki hoja kuondolewa. Kama Wabunge walio wengi watakubali, Spika, atasema "Hoja inaondolewa kwa idhini ya Bunge" Hapo hoja hiyo itakuwa imeondolewa na Bunge litaendelea na shughuh inayofuata.